

# Karibu!

Shelburne Farms ni shirika la elimu lisilo la faida linalofanya kazi ya kuhamasisha na kujenga maisha bora endelevu kupitia programu zetu, eneo letu, na bidhaa zetu. Tunatoa uzoefu wa kujifunza ili kuwasaidia walimu, wanafunzi, na wageni kama wewe kuunda dunia yenye ustawi zaidi.

Karibu kwenye eneo letu la kihistoria, shamba lenye ukubwa wa ekari 1,400. Mwanzoni mwa karne ya 20, eneo hili lilikuwa mali ya kilimo ya Lila Vanderbilt na William Seward Webb. Mwaka 1972, vizazi vya familia hii walianzisha shirika la elimu lisilo la faida hapa ili kusaidia kukabiliana na changamoto za kimazingira duniani. Eneo hili likawa darasa hai la kuleta hadithi za uendelevu katika uhalisia.

Kama Alama ya Kitaifa ya Kihistoria, shamba hili lipo kwenye ardhi jadi ambazo hazijawahi kupokonywa, ardhi za kitamaduni na za kisasa za kundi la Winooskik kutoka katika kabila la Waabenaki***.** Eneo hili limeunda—na pia limeundwa na—hadithi nyingi kwa muda mrefu. Hadithi za uendelevu, ukuaji, mabadiliko, na zaidi. Baadhi ya hadithi hizo zimeshirikishwa katika mwongozo huu, lakini unaweza kupata nyingine nyingi zaidi kwenye tovuti yetu. Ni hadithi zipi utakazogundua hapa na kuzipeleka nyumbani kwako? Na ni hadithi zipi za eneo unalotoka?

*Hii inamaanisha nini? Wa Abenaki hawakuwahi kisheria kukabidhi au kuuza ardhi yao kwa mtu yeyote; wao pamoja na mababu zao wameitunza ardhi hii kama ndugu zao kwa muda wote, na kundi la Winooskik kutoka katika kabila la Waabenaki bado linachukulia eneo hili kuwa nyumbani kwao hadi leo.




## Ramani ya Njia ya Shelburne Farms

*NYUMBA BINAFSI: Tafadhali heshimu faragha ya wakazi wa shamba na majirani. Kaa kwenye njia na uzingatie ishara zote za "faragha". Asante.*

*TAHADHARI: Njia zinaweza kuwa hazijatiwa alama, haziko sawa au ni telezi. Zingatia hali ya hewa, usiingie katika maeneo yenye uzio au kugusa uzio wa umeme na ulete maji. Kaa kwenye njia pale inapowezekana. Njia zinafungwa wakati wa machweo.*

*Kuwa mjanja kuhusu kupe: healthvermont.gov - Linda, Angalia, Ondoa, Tazama*

*Ziwa liko umbali wa maili 3½ kutoka Kituo cha Ukaribishaji. Hakuna basi.*

## Mambo muhimu



**1.Duka la Shamba & Kituo cha Kukaribisha Wageni**
Ziara yako inaanzia hapa. Eneo hili linaonyesha mazao na bidhaa kutoka kwenye shamba letu: jibini la cheddar (cheddar cheese), nyama, na sufu kutoka kwenye malisho yetu, sharubati ya maple kutoka kwenye msitu wa miti ya maple ya sukari, na mazao kutoka kwenye Bustani yetu ya Soko. Utapata pia bidhaa kutoka mashamba mengine ya Vermont. Duka hufunguliwa kila siku kuanzia saa 3:30 (saa tatu asubuhi) hadi 11:30 jioni. Hakikisha umejiandikisha ili kufahamu shughuli za siku hiyo.



**2. Jengo Kuu la Shamba (Farm Barn),** lenye ghorofa tano na uanja wa ndani wa ukubwa wa ekari mbili, ndilo kituo cha elimu na utawala cha shirika lisilo la faida. Lilijengwa kati ya mwaka 1886 na 1890 kama makao makuu ya shughuli za kilimo. Likiwa na ofisi; warsha za useremala, uchoraji, na udobi wa vyuma; sehemu za kuhifadhia vifaa, mazao, na vifaa vya kilimo; pamoja na banda la nyumbu. Jengo hili lilikarabatiwa mwaka 1991, likijumuisha pia saa yenye nyuso nne katika mnara wake, ambayo bado inahifadhiwa hadi leo, ikigonga` kila nusu saa na kila saa kamili.  Tazama upande wa nyuma kwa ramani ya jengo hili na maelezo kuhusu shughuli unazoweza kufanya hapa.



**3. Kilima cha Lone Tree (Lone Tree Hill)** Kikiwa ndiyo sehemu ya juu zaidi katika shamba hili, Kilima cha Lone Tree kinatoa mandhari nzuri upande wa magharibi, ukitazama shamba hili na Ziwa Champlain hadi Milima ya Adirondack katika jimbo la New York (Wawôbadenik, maana yake “milima myeupe” kwa lugha ya Abenaki). Hapa ndipo palipo na kumbukumbu ya Derick V. Webb, ambaye alitoa ardhi hii na majengo kwa shirika lisilo la faida mwaka 1984. Kilima cha Lone Tree hapo awali kilikuwa sehemu ya Shamba la Comstock (Comstock Farm), mojawapo ya mashamba madogo 32 yaliyokuwa yamenunuliwa na familia ya Webb katika miaka ya 1880 ili kuunda mashamba yao ya kilimo yenye ukubwa wa ekari 3,800.



**4. Lake Champlain** lina urefu wa maili 120 na upana wa maili 12 katika sehemu yake pana zaidi. Hadithi ya Abenaki inasema kwamba jitu Odzihozo alichimba ziwa hilo kwa kutumia mikono yake mikubwa, na kwa kufanya hivyo akaumba Milima ya Adirondacks na Green Mountains. Baadaye alijigeuza kuwa jiwe lijulikanalo kama Rock Dunder, linalopatikana kaskazini mwa Shelburne Point. Bonde la ziwa lina mito mikubwa 12 na vijito vingi vinavyochangia zaidi ya 90% ya maji ya ziwa hilo, ambayo hutegemewa na watu takriban 200,000 kwa matumizi ya kunywa. Je, maji unayokunywa yanatoka wapi ?

## Sehemu Nyingine Unazoweza Kupitia Katika Matembezi yako



**Ng’ombe wa aina ya Brown Swiss & Maziwa**
Mara mbili kwa siku, tunakamua takriban ng’ombe 110 wa aina ya Brown Swiss wenye damu safi. Kwa kuwa na kiasi kizuri cha mafuta ya siagi na protini, maziwa yao hutumika kutengeneza jibini la cheddar la hali ya juu, ambalo tunalitengeneza hapa. Ili ng’ombe atoe maziwa, huzalishwa kila mwaka ili kujifungua ndama. Ng’ombe wanaokamuliwa hupewa malisho bora yaliyo karibu na banda la kukamulia. Ndama wa kike (heifers) na ng’ombe wasio kamuliwa hulishwa mahali tofauti. Pia tunafuga ng’ombe wa mchanganyiko kwa ajili ya nyama. Programu yenye ufikiaji wa maziwa tu.



**Kondoo**
Tunafuga kondoo kwa ajili ya nyama na sufu (manyoya yao), na mara nyingi utaona kundi letu likilisha majani. Tuna aina tofauti za kondoo: Dorset, Border Leicester, na Navajo Churro.  Je, unaweza kubaini kondoo wa Churro kwa manyoya yao marefu yaliyosambaa?



**Sugarbush (msitu wa miti ya maple)**
Tunasimamia kwa njia endelevu ekari 400 za misitu, ikiwemo msitu wa miti ya maple (sugarbush) wenye karibu matundu 2,300 za kuchotea. Mwishoni mwa majira ya baridi, tunapiga tundu miti ya maple ya sukari ili kukusanya maji matamu, yanayopita kwenye mabomba ya buluu hadi kwenye njia kuu ya ukusanyaji na hatimaye kufika kwenye nyumba ya kutengeneza sharubati (sugarhouse). Huko, maji hayo yanachemshwa hadi kubadilika kuwa sharubati(syrup) tamu ya maple.  Galoni 40 za maji matamu ya maple = galoni 1 ya sharubati(syrup).




**Bustani za Maua za Kifahari**
Zikiwa kati ya Ziwa Champlain na Inn, bustani hizi zilikuwa shauku ya maisha ya muundaji wake, Lila Webb, ambaye aliziboresha na kuzitanua kuanzia mwaka 1898 hadi alipofariki mwaka 1936. Leo hii, baada ya juhudi kubwa za ukarabati, ni mfano bora wa bustani ya Kimarekani kwa ajili ya starehe yako, pamoja na mandhari yake ya kuvutia kuelekea ziwani.  Kumbuka: Bustani hizi ziko umbali wa maili 4 kwenda na kurudi kutoka Kituo cha Kukaribisha, na hakuna usafiri wa basi au gari ya kuwachukua wageni.

**Coach Barn (Banda la magari ya farasi)**
Nyumba ya Taasisi ya Shelburne Farms kwa Ajili ya Shule Endelevu, banda hili sasa hutumika kwa warsha na matukio ya kijamii, ingawa hapo awali lilikuwa ghala la magari ya farasi, sleji(sleighs), na farasi wenyewe. Kila majira ya joto, banda hili huwa na uhai tena wakati walimu wanajifunza jinsi ya kuwahamasisha wanafunzi wao kushiriki katika vitendo vya kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu.

**Market Garden** (**Bustani ya soko**)  Katika eneo ambalo hapo awali lilikuwa bustani na nyumba za kijani za mali hiyo, sasa kuna bustani yetu ya kilimo hai inayolima, mboga, maua, na matunda kwa ajili ya nyumba ya Inn, Duka la Shamba, na jamii ya eneo hilo. Mbinu zetu za kilimo—kubadilisha mazao, kupanda mazao ya kufunika ardhi, na kurudisha virutubisho kupitia utengenezaji wa komposti—huweka afya na tija ya udongo.



**Mandhari & Majengo**
Mtaalamu wa usanifu wa mandhari, Frederick Law Olmsted, Mzee, alitayarisha mipango ya awali ya mali hii mwaka 1887, akiigawa katika maeneo matatu: Shamba, Msitu, na Bustani. Aliacha alama yake pia katika maili za barabara za mzunguko zinazoficha na kuonyesha mandhari ya ziwa, nyasi, na majengo makubwa yaliyobuniwa na mtaalamu wa majengo Robert H. Robertson. Tafuta madirisha ya aina ya "umbo la nyusi(eyebrow)" kwenye paa la Jengo kuu la Shamba (Farm Barn), kipengele cha usanifu alichotumia mara nyingi.



**Kilima cha Windmill (Windmill Hill**)
Eneo hili liko katikati ya mandhari ya kazi ya shamba, na pia ni sehemu nyingine yenye mandhari ya kuvutia upande wa magharibi.

**Malisho na Mashamba (Pastures & Fields)**
Tunatumia mbinu ya kulisha mifugo kwa mpangilio: Ng'ombe zetu hulisha kwa muda mfupi lakini kwa nguvu katika eneo dogo la malisho, kisha wanahamishwa kwenda eneo jipya, na kutoa muda kwa nyasi ya eneo la malisho la awali kukua upya. Hii huimarisha mizizi minene na mimea yenye nguvu na lishe nzuri, huzuia mtiririko wa maji, huimarisha uhai wa viumbe vingi, ardhini, na huhifadhi kaboni. Pia tunavuna majani makavu (hay) na silaji(silage) kwa kutumia trekta. Katika mashamba yanayohifadhi ndege wa aina ya Bobolinks na Savannah Sparrows, tunapanga vema muda wa kuvuna majani makavu ili kuwapatia ndege hao nafasi ya kujenga viota na kuwalea ndege wachanga.

**Uwanja wa nyasi**   Tunaacha nyasi za bustani yetu zikue na tunatumia mashine za kukata nyasi zinazoendeshwa kwa umeme ili kupunguza utoaji wa kaboni kutoka kwa mafuta ya kisukuku (fossil fuels), kupunguza kelele na uchafuzi wa hewa, na kusaidia nyuki na wadudu wengine wa kupandisha mimea!

**Elimu Mwaka Mzima!**
Wanafunzi wa rika zote hushiriki katika masuala ya uendelevu katika kampasi yetu na nje yake. Mafunzo ya ardhi hii huanza hapa, lakini hayaishii hapa. Salimia makundi ya wanafunzi utakayoyaona wakati wa ziara yako. Kwa walimu hasa, tunayo:

Shelburne Farms
**Institute for Sustainable Schools**

Taasisi ya Shule Endelevu hutoa mafunzo ya kitaaluma kwa walimu, na ni matokeo ya huduma ya miaka 50 kwa walimu na shule. Inatoa programu na rasilimali za mabadiliko kwa walimu na wanafunzi kusaidia kuhamasisha kizazi kipya cha wabadilishaji wa jamii.   shelburnefarms.org/educators




## Ndani na Karibu na Jengo Kuu la Shamba (Farm Barn)

1. **Bustani ya Watoto ya Shamba** Tembelea wanyama wa shamba walioko ndani ya jengo la shamba na kwenye malisho yanayozunguka—kama vile kondoo, mbuzi, ng'ombe, sungura, na wengine zaidi—na furahia shughuli zilizopangwa kwa siku nzima.
2. **Beeken Parsons** Mafundi hawa wenye ujuzi hutumia mbao zinazotengenezewa hapa na sehemu nyingine kutengeneza samani nzuri.
3. **Farm Cart** (**Gari la Shambani**) linahudumia chakula kilicholimwa shambani. Ratiba hubadilika. changanua msimbo katika kisanduku cha "For Current Information" (Kwa Habari Za Sasa) upande wa kulia.
4. **Utengenezaji wa Jibini** Tazama na jifunze jinsi wafanyakazi wa kutengeneza jibini wanavyotengeneza jibini la cheddar kutoka kwa maziwa ya ng'ombe wetu wa aina ya Brown Swiss, na "Kutana na Mtengenezaji wa Jibini." Ratiba hubadilika.
5. **Kituo cha Elimu cha McClure** Programu zetu nyingi huanza hapa.
6. **O Bread Bakery** (chini ya baraza) ni kiwanda cha uzalishaji cha mikate na biskuti vya asili vinavyouzwa kwa wageni wa siku.

Trekta ya usafiri huenda kutoka Kituo cha Ukaribishaji hadi Banda la Shamba kwa nusu saa, saa 4 asubuhi hadi saa 10 jioni, kulingana na msimu.



**Sheep's Knoll (Kilima cha Kondoo)**
Tazama kuelekea mashariki kutoka kwenye Jengo la Shambani kuelekea Milima ya Green Vermont (Skanontkaraksèn:ke, "mahali penye miinuko isiyokuwa na mpangilio" kwa lugha ya Mohawk), na mlima mrefu zaidi wa Vermont, Mlima Mansfield wenye urefu wa futi 4,393. Unaona "kidevu" na "pua" kwenye uso wake mrefu? Kusini zaidi, kuna mlima Camel's Hump, au Dowabodiwadjo, "Mlima wa kiti cha Farasi (Saddle Mountain)" kwa lugha ya Abenaki, ambao labda ndiyo mlima unaotambulika zaidi Vermont.

**Paneli za Jua**
Je, unaweza kupata paneli 96 za jua zilizo juu ya paa la Jengo kuu la Shambani? Zinazalisha umeme kwa ajili ya mtandao wa Green Mountain Power. Vyanzo vya nishati ya jua vilivyo hapa shambani na nje ya shambani vinakidhi sehemu kubwa ya mahitaji yetu ya umeme kwa kutumia nishati mbadala. Hii ni mojawapo ya mikakati yetu ya kufikia lengo la kuwa na uzalishaji wa kaboni hasi ifikapo mwaka 2028—kukamata kaboni zaidi kwenye miti na udongo wetu kuliko ile inayotolewa na majengo na shughuli zetu.



## Nyumba ya wageni ya Shelburne Farms (Shelburne Farms Inn)

Furahia kulala usiku mmoja au kupata mlo katika nyumba ya kihistoria yenye vyumba 24 vya wageni. Ilijengwa kati ya 1887 na 1900 kama makazi ya Lila na Seward Webb, na ikageuzwa kuwa nyumba ya wageni mwaka 1987. Nyumba hii inakaribisha watu kupumzika na kupata msukumo kutoka eneo hili pamoja na malengo yake. shelburnefarms.org/inn

**Kwa taarifa za Sasa**
Kwa ratiba, tarehe, na maelezo ya hivi karibuni kuhusu huduma na shughuli zetu, changanua msimbo au tembelea tovuti yetu.
shelburnefarms.org/visit

**Gundua Kupitia Ziara!**
- Ziara ya Shelburne Farms
- Ziara ya Jua hadi Jibini (Sun to Cheese Tour)
- Ziara ya Nyumba na Bustani (House & Garden Tour) . changanua msimbo au tembelea: shelburnefarms.org/calendar

## Saidia Shelburne Farms

Inahitaji rasilimali kubwa sana za kifedha kutunza na kushiriki eneo hili la ajabu na kila mtu. Kama shirika la elimu lisilo la faida, tunategemea wewe! Jiunge nasi kama msaidizi leo!
Zawadi zote zinathaminiwa. Asante sana!

Picha: Daria Bishop, Holly Brough, Andrea Estey, Brent Harrewyn, Jared Vincent, Marshall Webb, Sarah Webb